# TANGAZO TANGAZO
# OFISI YA MKUU WA WILAYA RUFIJI INAWATANGAZIA VIJANA WOTE WENYE SIFA KUJIUNGA NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (JKT) KWA UTARATIBU WA KUJITOLEA (HIARI) KWA MWAKA 2022/2023

**MUOMBAJI AWE NA SIFA ZIFUATAZO:-**

1. Awe raia wa Tanzania.
2. Umri:
   a) Kwa vijana wenye elimu ya darasa la saba umri ni kuanzia miaka 16 hadi 18
   b) Vijana wenye elimu Kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka 20.
   c) Vijana wenye elimu Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka 22.
   d) Vijana wenye elimu ya stashahada umri usiwe zaidi ya miaka 25
   e) Vijana wenye elimu ya shahada umri usiwe zaidi ya miaka 26
   f) Vijana wenye elimu ya shahada ya uzamivu umri usiwe zaidi ya miaka 30
   g) Vijana wenye elimu ya shahada ya uzamivu umri usiwe zaidi ya miaka 35.
3. Awe na afya njema, akili timamu na asiwe na alama yeyote ya michoro mwilini (Tattoo).
4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.

5. Kwa vijana waliomaliza elimu ya sekondari kidato cha nne na sita wawe waliomaliza kuanzia 2019, 2020, 2021 na 2022 wenye ufaulu ufuatao:-
    a. Wawe wamefaulu na wawe na alama (Points) zisizopungua 32.
    b. Vijana Kidato cha sita wawe na ufaulu wa daraja la kwanza hadi daraja la nne.
6. Awe na elimu ya msingi aliyehitimu darasa la saba
7. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate)
8. Awe na cheti halisi cha kumaliza shule (School Leaving Certificate)
9. Awe na Cheti halisi cha matokeo (Original Academic Certificate/Transcript).
10. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au KMKM wala kuajiriwa na Idara nyingine serikalini.
11. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma.
12. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yana yofanana na hayo.
13. Kwa wale wenye vipaji vya michezo mbalimbali na sanaa sifa za elimu ni Sawa na zilizojatwa hapo juu.

Maombi yote yawasilishwe; kwa anuani:-

**Ofisi ya Mkuu wa Wilaya,**
**S. L. P 1,**
**UTETE/RUFIJI**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 3/09/2022 saa 10:00 Jioni na usaili utafanyika tarehe 4/9/2022 kuanzia saa 2:00 Asubuhi.**